



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



MWALIKO WA WATAZAMAJI WA NDANI WA  
UCHAGUZI MDOGO JIMBO LA KONDE MKOA WA KASKAZINI PEMBA -  
ZANZIBAR NA KATA SITA ZA TANZANIA BARA

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Konde, Mkoa wa Kaskazini Pemba- Zanzibar tarehe 18 Julai, 2021. Kwa mujibu wa kanuni ya 18 (3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 16(3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za mwaka 2020, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepewa mamlaka ya kualika na kusajili watazamaji wa uchaguzi wanaotaka kutazama uchaguzi.

Kupitia tangazo hili, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inapenda kualika Taasisi na Asasi mbalimbali nchini ambazo zinahitaji kutazama uchaguzi mdogo katika Jimbo la Konde na Kata sita za Tanzania Bara. Asasi na Taasisi zenye nia ya kutazama uchaguzi huo zinatakiwa kuwasilisha maombi kwa kutumia Mfumo wa Menejimenti ya Watazamaji (OMS) kupitia "*link*" ifuatayo <https://oms.nec.go.tz>.

Barua ya maombi pamoja na mambo mengine itatakiwa kuainisha mambo yafuatayo-

- i. Anuani kamili ya Taasisi au Asasi husika;
- ii. Mahali ambapo Taasisi au Asasi husika inafanyia kazi (Physical address);
- iii. Shughuli ambazo zinafanywa na Taasisi au Asasi husika kwa mujibu wa hati ya usajili;
- iv. Sehemu ambazo Taasisi au Asasi inataka kufanya zoezi hilo la utazamaji;
- v. Idadi ya watu ambao Taasisi au Asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na taarifa zao;
- vi. Majina na namba za simu za viongozi wa Taasisi au Asasi husika kama yalivyoandikwa katika hati za usajili wa Taasisi au Asasi;

- vii. Ikiwa Taasisi au Asasi inahusisha watendaji wa kimataifa, wawili lazima wawe Watanzania;
- viii. Kuambatisha nakala au kivuli cha hati ya usajili wa Taasisi au Asasi husika; na
- ix. Kuambatisha nakala au kivuli cha katiba ya Taasisi au Asasi husika.

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 20 Juni, 2021.**

Imetolewa leo tarehe 11/6/2021 na:

  
Dkt. Wilson Mahera Charles

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**